**MHESHIMIWA DR. SAMIA SULUHU HASSAN AONYESHA NIA YA TANZANIA KUJIUNGA TENA NA OGP**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya **Mheshimiwa Rais Dr. Samia Suluhu Hassan** kwa kufikiria tena kujiunga na Mpango wa Ubia wa Serikali Huria yaani *Open Government Partnership* kama jukwaa kuendelea kuboresha hali ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Utawala bora nchini kwa manufaa mapana ya watanzania na kuhakikisha kwa pamoja tunapeleka mbele ajenda za maendeleo ya watanzania na taifa kwa ujumla. Tunatambua pia jitahada zilizofanywa na viongozi mbalimbali wakiwemo mawaziri katika kushawishi umuhimu wa Tanzania kujiunga ten ana OGP.

Mwishoni mwa mwaka 2022, THRDC ilitoa Waraka wa kuishauri Serikali yetu kuhusu umuhimu wa kujiunga tena na OGP. Tanzania ilijiunga na OGP mwaka 2011 na kujiondoa mwaka 2017. Kipekee tunaipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kujiunga tena na OGP kama ambavyo Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan alivyothibitisha wakati akihutubia Mkutano wa Demokrasia tarehe 29/03/2023 uliofanyika kwa njia ya Mtandao.

> "*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kuunga mkono demokrasia, haki za binadamu na utawala bora ndani na nje ya nchi, na tunatazmia kurudi kwenye Mpango wa Ubia wa Serikali Huria yaani (OGP)….demokrasia inaweza tu kustawi pale haki za binadamu zinapoheshimiwa, na sheria zinazingatiwa. Serikali yetu imeupa kipaumbele kikubwa ukuzaji wa haki za binadamu nchini na vizuizi vya utimilifu wa haki za binadamu vimeondolewa.*" Mh. Dk. Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia Mkutano wa Demokrasia tarehe 29/03/2023.

Ni ukweli usiopingika kuwa Salamu hii imebeba maana na uhalisia wa dhana ya Mheshimiwa Rais ya **4Rs** ikiwemo *Rebuilding yaani kujenga upya* na *Reforms ikimaanisha maboresho*. Hii ni kutokana na mambo mazuri yanayofanywa na Serikali chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haki za binadamu na utawala wa sheria ndiyo misingi ya maendeleo ya nchi yoyote ile duniani. Watetezi wa haki za binadamu jukumu letu ni kulinda haki za binadamu, kokosa na kuishauri serikali katika mambo mbalimbali. Kwa Tanzania kujiunga tena OGP itasaidia kutuongoza katika misingi ya utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na utawala bora. Misingi hii ndiyo nguzo za maendeleo katika nchi yoyote ile duniani.

Nia ya Serikali kujiunga tena na OGP ni nia njema katika kuleta mabadiliko chanya kisheria na kitaasisi nchini Tanzania. Tanzania itafaidika na mamabo mbalimbali kwa kujiunga tena na OGP kama ifuatavyo;

1. OGP imejengwa katika misingi mikuu ya utawala bora ambayo ni, uwazi, ushirikishwaji wa wananchi, uwajibikaji na uadilifu na teknolojia na ubunifu ambao unaonekana kuwa mwelekeo wa sasa wa uongozi wa Serikali ya awamu ya sita. Ulinzi wa haki za binadamu na upatikanaji wa haki unakua imara zaidi pale ambapo misingi hii inazingatiwa.
2. Mpango wa Sasa wa Maendeleo wa Miaka Mitano unasisitiza juu ya ushirikishwaji na ushiriki wa wananchi katika programu mbalimbali za maendeleo. OGP ni chombo chenye nguvu cha kufikia vipaumbele vya nchi nzima kwa Serikali ya Tanzania na Asasi za Kiraia.
3. Katika ngazi ya kitaifa, jukwaa la OGP linaweza kutumika kama njia inayopatikana kwa urahisi, inayomilikiwa na nchi kwa pamoja ili kuleta mageuzi madhubuti ambayo yatakuwa sehemu ya Mpango Kazi wa OGP wa Tanzania.
4. Katika ngazi ya kimataifa, OGP inaweza kusaidia kutoa jukwaa la kikanda na kimataifa ili kuonyesha na kukuza juhudi za wazi za serikali ya Tanzania, na jukwaa la kubadilishana uzoefu na serikali nyingine na asasi za kiraia kote Afrika na kwingineko.
5. OGP inaunda jukwaa thabiti la kuendeleza na kutekeleza mabadiliko ya ndani na sera za serikali wazi. OGP inatoa mfumo wa hatua imara katika kushinikiza masuala ya sera ya umma katika ngazi ya kitaifa. Kwa mfano, ahadi za OGP zinaweza kuzingatia; kufanya huduma za za kijamii kuwa za manufaa na ufanisi zaidi; kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia uvumbuzi na uwazi; kupambana na rushwa; kutumia teknolojia kuifanya serikali iwe wazi zaidi na sikivu kwa wananchi; na mengi zaidi. Hii inazipa nafasi asasi za kiraia kushauri na kushiriki katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi.
6. OGP inaweza kutoa mchango wa kimawazo, utaalamu, zana, na majukwaa ya kusaidia serikali kufafanua utashi wa kisiasa katika maboresho na kuimarisha programu zinazotekelezeka kwa kuwashirikisha wadau zikiwemo AZAKI na watetezi wa haki za binadamu.
7. OGP pia inaweza kutumika kama njia ya kuunganisha na kuratibu maboresho mbalimbali ya utawala bora katika wizara na mashirika mbalimbali huku ikikusanya na kuwasilisha shuhuda za jinsi ahadi za OGP zimeleta mabadiliko katika sekta mbalimbali.
8. OGP inasaidia kuanzisha midahalo kwa ajili ya utatuzi wa matatizo ya pamoja kwenye nchi shiriki, kuhamisha tawala za umma kuelekea utamaduni wa utungaji sera ulio wazi zaidi na shirikishi, na kuboresha huduma za serikali kwa watu.
9. OGP inatoa fursa bora za kubadilishana na kuwezeshana mbinu bora za kiutendaji. Kwa mfano, katika ngazi ya kimataifa, OGP hutoa fursa ya jukwaa la kimataifa kuunganisha, kuwezesha, kutambua na kusaidia wanamageuzi wa ndani waliojitolea kubadilisha serikali na jamii kupitia uwazi na ushirikishwaji. OGP huwatia moyo wana mabadiliko, hutoa nafasi salama kwa ajili ya kujadili changamoto zinazofanana, hutumika kama jukwaa la utatuzi wa matatizo ya

pamoja, na kuimarisha hisia za jumuiya miongoni mwa wanamageuzi wanaofanya kazi kuboresha tawala zao za umma.

10. OGP inakuza kutambuliwa kimataifa na inatoa fursa ya kuonyesha mafanikio ya mabadiliko ya Tanzania kupitia mawasilisho yanayofanywa na Serikali Pamoja na AZAKI.
11. OGP inakuza nafasi ya kijamii na makundi ya kijamii kushiriki kwa uwazi katika mipango mbalimbali ya nchi.

Tunaamini jukumu letu kama AZAKI na watetezi wa haki za binadamu wa nchi hii ni kuishauri serikali ipasavyo kuhusu suala lolote la maslahi ya umma. Tunaamini kwamba AZAKi na watetezi wa haki za binadamu ni washirika bora wa serikali katika kuendeleza utamaduni wa haki za binadamu, utawala bora na maendeleo endelevu. THRDC inawashauri wanachama wake wote Pamoja na AZAKI zingine kuanza kuwa tayari kushirikiana katika kujenga ushirika imara wa watetezi wa haki za binadamu katika kuratibu maswala la OGP kwa upade sekta ya AZAKI hapa Tazania. THRDC pia inawakumbusha wanachama wake kuendelea kutetea haki za binadamu bila woga na kwa kuzingatia sheria na maadili na tamaduni za Kitanzania.

**Imetolewa na;**
**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**
**31/03/2022**